# Jinsi ya Kukata Rufaa Dhidi ya Uamuzi wa WIC

## Haki za Kukata Rufaa na Muhtasari

Ikiwa mpango wa WIC utakosa kusajili wewe/mtoto wako au ukikuondoa wewe/mtoto wako na uhisi uamuzi huo haukuwa wa haki, una haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo. Una siku 60 kuanzia tarehe utakayojulishwa kuhusu uamuzi wa kuomba kusikilizwa kwa haki. Ikiwa siku 60 zimepita, hupaswi kuomba usikilizaji wa kesi. Unaweza kuwasilisha ombi lako bila hofu kuwa utasumbuliwa au kuadhibiwa. Taarifa kuhusu usikilizaji wa haki inapatikana katika tovuti zote za WIC na katika **tovuti ya Idara ya Afya ya Vermont.**

https://www.healthvermont.gov/family/wic/usda-nondiscrimination-statement#wicappeals

Ikiwa umenyimwa msaada wa WIC kutokana na ukiukaji wa mshiriki na ulijulishwa kwa barua, ombi lako la Usikilizaji wa Haki lazima liwasilishwe ndani ya siku sitini (60) kuanzia tarehe iliyo kwenye stempu za posta za barua ya uamuzi huo au tarehe ulipojulishwa kuhusu uamuzi huo kwa barua.

Vikao vya Usikilizaji wa Haki hufanywa na Bodi ya Huduma za Kibinadamu (HSB) ya Shirika la Huduma za Kibinadamu la Vermont. Unaweza kuwasilisha ombi la Usikilizaji wa Haki ana kwa ana, kwa simu, au kwa barua au barua pepe kwa Jimbo au shirika la eneo lako. Huduma za tafsiri zitatolewa na taarifa kuhusu rufaa zinaweza kuombwa katika lugha zingine (Kialbania, Kiarabu, Kiburma, Kidari, Kifaransa, Kirundi, Kinepali, Kipashto, Kichina Sahili, Kisomali, Kihispania, Kiswahili, Kichina cha Jadi, Kivietinamu).

## Jinsi ya Kuomba Usikilizaji wa Kesi

Maombi ya rufaa ya Usikilizaji wa Haki na/au Mikutano Katika Ofisi ya Eneo yanaweza kuwasilishwa ana kwa ana, kwa simu, barua au barua pepe kwa Ofisi ya WIC ya Jimbo, Bodi ya Huduma za Kibinadamu au ofisi ya WIC ya eneo lako. Jaza **Fomu ya Rufaa** kwa kila ombi la Usikilizaji wa Haki na/au Mkutano Katika Ofisi ya Eneo. Fomu ya rufaa inapatikana katika miundo ya karatasi na ya kielektroniki. Ombi lako linapowasilishwa ana kwa ana, nakala ya karatasi ya fomu hiyo itatolewa. Ikiwa unahitaji usaidizi wa kujaza fomu, unaweza kuomba usaidizi na kuwaomba wafanyakazi watengeneze nakala na kutuma fomu ya karatasi kwa barua pepe kwa WIC@Vermont.gov (barua pepe ya Ofisi ya WIC ya Jimbo) na Bodi ya Huduma za Kibinadamu (HSB) kwa contact.hsb@vermont.gov.

Ukijaza fomu ya kielektroniki ya rufaa, unapaswa kuhifadhi nakala kwenye kompyuta yako na ama uitume kwa barua pepe kwa anwani zilizo hapo juu au kwa barua kwa Mkurugenzi wa WIC wa Jimbo:

State WIC Director
Vermont WIC Program
280 State Drive
Waterbury, VT 05671-8360

## Je, Usikilizaji wa Haki ni nini?

Katika kikao cha **Usikilizaji wa Haki** , unaweza kuuliza maswali na kueleza kwa maneno yako mwenyewe kwa nini unahisi uamuzi huo si sahihi au si wa haki. Unaweza kuchagua kujiwakilisha au unaweza kuchagua mtu mwingine akuwakilishe, kama vile jamaa, rafiki, wakili au msemaji mwingine.

Unaweza pia kuomba Mkutano Katika Ofisi ya Eneo. Unaweza kuomba Mkutano Katika Ofisi ya Eneo wakati wowote, ikiwemo wakati ule ule unapoomba Usikilizaji wa Haki**.** Mkutano Katika Ofisi ya Eneo si wa lazima. Mkutano Katika Ofisi ya Eneo ni mkutano kati yako, msimamizi wa ofisi ya eneo na mkurugenzi au mwakilishi wa WIC ya Jimbo. Unaweza kuchagua kuleta mwakilishi, kama vile jamaa, rafiki, mwanasheria au msemaji mwingine kwenye Mkutano Katika Ofisi ya Eneo. Mkutano Katika Ofisi ya Eneo utafanyika ndani ya siku 10 za kazi baada ya ombi lako katika ofisi ya WIC ya eneo lako au kwa mkutano wa video. Mkutano Katika Ofisi ya Eneo unaweza kukuwezesha kutatua suala hilo kabla ya Usikilizaji wa Haki kufanyika au kukamilika. Ikiwa hutaki Mkutano Katika Ofisi ya Eneo au hujaridhishwa na matokeo ya Mkutano Katika Ofisi ya Eneo, unaweza kuomba Usikilizaji wa Haki.

**Ombi lako la Usikilizaji wa Haki wa Kesi linaweza kukataliwa ikiwa:**

1) Utakosa kuwasilisha ombi lako la Usikilizaji wa Haki ndani ya siku sitini (60);
2) Wewe au mwakilishi wako ataondoa ombi lako la Usikilizaji wa Haki kwa maandishi;
3) Wewe au mwakilishi wako, bila kutoa sababu nzuri, atakosa kufika kwenye kikao cha Usikilizaji wa Haki; au
4) Ulinyimwa ushiriki katika Usikilizaji wa Haki uliofanywa hapo awali na huwezi kutoa ushahidi kwamba hali zako zinazohusiana na ustahiki wako au wa mtoto wako zimebadilika kwa njia ambayo inahalalisha Usikilizaji mwingine wa Haki.

**Taarifa ya Matokeo ya Rufaa**

HSB lazima ikujulishe kwa maandishi kuhusu uamuzi ndani ya siku 45 baada ya kuambia WIC kuwa ulitaka usikilizaji wa haki. HBS ikiamua kwamba unapaswa kupata msaada, msaada huo lazima uanze kutolewa mara moja. Utakuwa na fursa ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu katika Mahakama ya Juu ya Vermont.

**Ikiwa unahitaji taarifa zaidi au una maswali, unaweza kupiga simu kwa Ofisi ya WIC ya Jimbo la Vermont kwa 1-800-649-4357 au Bodi ya Huduma za Kibinadamu kwa 802-828-2536.**

# Fomu ya Rufaa ya WIC

## Mpango wa WIC wa Idara ya Afya ya Vermont

Tafadhali jaza fomu hii ili kuomba Mkutano Katika Ofisi ya Eneo, Usikilizaji wa Haki, au yote mawili.

Ikiwa unahitaji taarifa zaidi au una maswali, unaweza kupiga simu kwa Ofisi ya WIC ya Jimbo la Vermont kwa 1-800-649-4357 au Bodi ya Huduma za Kibinadamu kwa 802-828-2536.

1. Ninaomba jambo lifuatalo, kama ilivyoelezwa katika kanuni za Mpango wa WIC:

   ☐ **Mkutano Katika Ofisi ya Eneo**

   ☐ **Usikilizaji wa Haki**

   ☐ **Yote Mawili**

2. Tafadhali eleza, kwa maneno yako mwenyewe, kwa nini unahisi uamuzi wa kukunyima msaada wa WIC si sahihi au si wa haki kulingana na viwango vya ustahiki vya WIC.

3. Jina Kamili
(La Kwanza, Herufi ya Kwanza ya Jina la Kati, La Mwisho) ____________________________________________

4. Anwani ya Barua: ____________________________________________

5. Barua Pepe: ____________________________________________

6. Nambari ya Simu: ____________________________________________

7. Ikiwa unaomba usikilizaji wa haki kwa niaba ya watoto katika familia yako ambao wamenyimwa msaada wa WIC, tafadhali andika majina yao kamili na tarehe ya(za) kuzaliwa hapa chini.

Jina Kamili: ______________________________ Tarehe ya kuzaliwa: ______________

Jina Kamili: ______________________________ Tarehe ya kuzaliwa: ______________

Jina Kamili: ______________________________ Tarehe ya kuzaliwa: ______________

Jina Kamili: ______________________________ Tarehe ya kuzaliwa: ______________

7. Ikiwa ungependa kuleta mwakilishi wa kuhudhuria kikao cha usikilizaji wa kesi nawe, tafadhali andika jina lake, anwani, barua pepe na/au nambari yake ya simu.

Jina: ____________________________________________

Anwani: ____________________________________________

Barua Pepe: ____________________________________________

Simu: ____________________________________________

8. Je, ungependa mkalimani au mtafsiri awepo kwenye kikao cha usikilizaji wa kesi? ☐ Ndiyo ☐ Hapana

7. Ikiwa ndiyo, lugha inayohitajika ni: ____________________________________________

8. Tarehe ilipojazwa: ____________________________________________

Jaza fomu, uihifadhi na uitume kwa barua kwa Mkurugenzi wa WIC:

State WIC Director
Vermont WIC Program
280 State Drive
Waterbury, VT  05671-8360

Au, unaweza kuihifadhi na utume fomu kwa barua pepe kwa WIC@Vermont.gov (barua pepe ya Ofisi ya WIC ya Jimbo) na/au Bodi ya Huduma za Kibinadamu kwa contact.hsb@vermont.gov.

Shirika hili ni mtoa huduma sawa kwa wote.

**Kwa mipango mingine yote ya misaada ya lishe ya FNS, mashirika ya jimbo au ya eneo, na wakandarasi wake wadogo, lazima wachapishe Taarifa ifuatayo ya Kutobagua:**

Kwa mujibu wa sheria ya shirikisho ya haki za kiraia na sheria na sera za haki za kiraia za Idara ya Kilimo ya Marekani (USDA), taasisi hii hairuhusiwi kubagua kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, jinsia (ikiwa ni pamoja na utambulisho wa kijinsia na mwelekeo wa kijinsia), ulemavu, umri, au kulipiza kisasi kwa kuhusika katika shughuli za awali za haki za kiraia.

Maelezo ya mpango yanaweza kupatikana katika lugha zingine isipokuwa Kiingereza. Watu wenye ulemavu wanaohitaji njia mbadala za mawasiliano ili kupata maelezo ya mpango (km, Breli, maandishi makubwa, kanda ya sauti, Lugha ya Ishara ya Marekani), wanapaswa kuwasiliana na Shirika husika la Jimbo au la eneo linalotoa mpango au Kituo cha TARGET cha USDA katika (202) 720-2600 (sauti na TTY) au wawasiliane na USDA kupitia Huduma ya Uelekezi ya Shirikisho (Federal Relay Service) katika (800) 877-8339.

Ili kuwasilisha malalamiko ya ubaguzi katika mpango, Mlalamishi anapaswa kujaza Fomu ya AD-3027, Fomu ya Malalamiko ya Ubaguzi wa Mpango wa USDA ambayo inaweza kupatikana mtandaoni katika: https://www.fns.usda.gov/sites/default/files/resource-files/ad3027-swahili.pdf, au kutoka ofisi yoyote ya USDA, kwa kupiga simu (866)-632-9992, au kwa kutuma barua kwa USDA. Barua lazima ijumuishe jina, anwani, nambari ya simu ya mlalamishi, na maelezo ya maandishi ya madai ya kitendo cha ubaguzi kwa undani wa kutosha ili kumfahamisha Katibu Msaidizi wa Haki za Kiraia (ASCR) kuhusu asili na tarehe ya madai ya ukiukaji wa haki za kiraia. Fomu au barua iliyojazwa ya AD-3027 lazima iwasilishwe kwa USDA kupitia:

**(1)** **barua:**
U.S. Department of Agriculture
Office of the Assistant Secretary for Civil Rights
1400 Independence Avenue, SW
Washington, D.C. 20250-9410; au

**(2)** **faksi:**
(833) 256-1665 au (202) 690-7442; au

**(3)** **barua pepe:**
program.intake@usda.gov

Taasisi hii ni mtoa huduma asiyebagua.